



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

BARAZA LA TAIFA LA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

(NEMC)



**KUFUTA USAJILI WA MIRADI ILIYOSAJILIWA KWA NJIA YA NAKALA
NGUMU KWAAJILI YA MCHAKATO WA TATHMINI YA ATHATI KWA
MAZINGIRA (EIA) NA UKAGUZI WA MAZINGIRA (EA)**

1. Kanuni ya 41A ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi) zilizofanyiwa maboresho mwaka 2018 kinaelekeza kuwa "Uhalali wa nyaraka za miradi zilizowasilishwa Baraza kwaajili ya kupata Cheti cha Mazingira utakuwa ni miaka miwili na baada ya muda huo kuisha, Baraza linaweza kufuta usajili wa maombi hayo". Kanuni imelipa Baraza mamlaka hayo ya kufuta miradi ambayo imekaa kipindi cha zaidi ya miaka miwili bila kumaliza mchakato wa EIA/EA.
2. Baraza linawataarifu wawekezaji wote ambao walisajili miradi yao kwaajili ya mchato wa EIA/EA na hawakukamilisha mchakato huo ndani ya muda uliotajwa kuwa miradi hiyo imefutwa usajili kuanzia tarehe 13/02/2023. Kwahiyo Baraza halitapokea nyaraka zozote zinazohusiana na uendelezaji/ukamilishaji wa maombi ya miradi hiyo ambayo orodha yake imeanishwa katika tangazo hili.
3. Hata hivyo mwekezaji anaweza kusajili upya mradi wake na kuanza mchakato wa EIA/EA kupitia mfumo wa usajili wa miradi kielektroniki eia.nemc.or.tz.

Limetolewa na: Eng. Dkt. Samuel G. Mafwenga

MKURUGENZI MKUU